TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI - SEPTEMBA, 2017

1.0 UTANGULIZI:

Taarifa hii ni ya mapato na matumizi kwa kipindi cha mwezi Septemba, 2017. Eneo la mapato limeonyesha mapato ya ndani na ya nje. Upande wa matumizi imeonyesha matumizi katika maeneo ya mishahara na matumizi ya kawaida pamoja na maendeleo.

1.1 MAPATO:

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba, 2017 Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni imekusanya na kupokea jumla ya **TZS. 3,979,849,396.00** kati ya makisio yenye jumla ya **TZS. 36,333,575,000.00.** Mapato hayo ni sawa na **11%** ya makisio. Kati ya makisio hayo kiasi cha **TZS. 9,218,868,000.00** ni mapato ya ndani (Council Own Source) na **TZS. 27,114,707,000.00** ni ruzuku kutoka Serikali kuu, mifuko ya pamoja, wafadhili mbalimbali na nguvu za wananchi.

- Hata hivyo katika kipindi cha **Julai** - **Septemba, 2017** Mapato ya vyanzo vya ndani ni **TZS. 1,057,845,296.00** sawa na **11%** ya lengo la **TZS. 9,218,868,000.00** na vyanzo vya nje tumepokea **TZS. 2,922,004,100.00** ambayo ni **11%** ya lengo la **TZS. 27,114,707,000.00**.

1.2 MAPATO YA NDANI:

Kama **jedwali Na.1** linavyoonesha **Julai** - **Septemba, 2017** kiasi cha mapato ya ndani kilichokusanywa.
Hata hivyo vipo vyanzo ambavyo kwa kiasi kikubwa vitaendelea kuathiri bajeti yetu kutokana na sababu mbalimbali kama ifuatavyo:-

1.2.1 KODI YA MAJENGO:

Chanzo hiki kina bajeti ya **TZS.1,000,000,000.00** ambapo kuanzia Agosti, 2016 chanzo hiki kimekuwa kikikusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania **(TRA).** Wakati wa Bajeti tulikiondoa lakini tukaelekezwa kukiacha kwa maelezo kuwa, pamoja na kukusanywa na TRA bado matumizi yake yataendelea kuwa kwetu. Mwisho wa mwaka 2016/2017 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilirejesha kiasi cha fedha **TZS.398,704,356.00** kwa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke. Tumefanya mawasiliano na Temeke kwa barua yenye Kumb Na. **AB.31/386/01/39 ya tarehe 15/08/2017** ili watupatie mgao wetu wa **40%** ambazo ni sawa na **TZS. 159,481,742.40.**

Pia tumeandika barua kwa Katibu Tawala (M) ili kusaidia urejeshwaji wa fedha hizo kwa barua yenye Kumb. Na. AB.31/386/01/40 ya tarehe 11/09/2017 na nakala kwa Katibu Mkuu TAMISEMI.

1.2.2 USHURU WA MABANGO:

Chanzo hiki kina bajeti ya **TZS. 600,000,000.00** ambapo kuanzia Julai, 2017 chanzo hiki kinakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Maelezo ya ziada ni kama ilivyo kwenye Kodi ya majengo.

Jedwali Na 1: MUHTASARI WA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI - SEPT, 2017

MAELEZO	MAKISIO 2017/2018	Jul - Ags,2017	Septemba, 2017	Jul - Sept, 2017	%
Vyanzo vya ndani (own source)	9,218,868,000.00	667,191,883.00	390,653,413.00	1,057,845,296.00	11
Vyanzo vya nje (External Source)	27,114,707,000.00	1,478,285,400.00	730,745,600.00	2,922,004,100.00	11
JUMLA	36,333,575,000	2,142,307,283.00	1,121,399,013.00	3,979,849,396.00	11

2.0 CHANGAMOTO:

- Baadhi ya vyanzo vya mapato kukusanywa na mamlaka nyingine wakati matumizi yake yamepangwa kufanyika kwetu, kama vile kodi ya majengo, ushuru wa mabango na kodi ya ardhi ambavyo huathiri utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Halmashauri.
- Serikali Kuu kuchelewa kutoa ruzuku kwa ajili ya shughuli mbalimbali za jamii ya Kigamboni ambapo Halmashauri inaelemewa na majukumu mazito kama vile gharama za uendeshaji Mitihani ya Taifa kuanzia Darasa la Pili, Nne, Saba, Kidato cha Pili, Nne na Sita nakadhalika. Hivi sasa maandalizi ya mitihani ya kidato cha nne yanaendelea na mahitaji ya rasilimali fedha ni makubwa.
- Utekelezaji wa maelekezo toka Serikali kuu nje ya bajeti. Kwa mfano shule ya Sekondari Nguva na ujenzi wa majengo ya ofisi za utawala kwa idara za Elimu ni changamoto kubwa kwa Halmashauri yetu.

3.0 MKAKATI WA UKUSANYAJI MAPATO:

Halmashauri imejizatiti kuboresha ukusanyaji wa mapato kwa kufanya yafuatayo:-

- Halmashauri itaendelea kuboresha mikakati ya kuongeza mapato ya ndani na uwezo wa kujitegemea baada ya kupitishwa kwa sheria mpya za Halmashauri yetu.
- Kuendelea kuingiza takwimu za walipa kodi wapya na kuboresha takwimu za walipa kodi waliopo kwenye mfumo wa **GIS** na **LGRCIS.**

- Kufanya ukaguzi na ulinganifu wa taarifa za wakaguzi kwa walipa ushuru wa huduma (service levy) ili kubaini kama wanalipa kiasi stahili.
- Kuendelea kukamilisha mfumo wa kieletroniki kwa kukusanya mapato katika vituo vya Afya na Hospitali za Halmashauri ili kuepuka uvujaji wa mapato ya uchangiaji kwenye huduma za Afya.
- Idara ya ujenzi kwa kushirikiana na idara ya mipangomiji kufanya ukaguzi wa majengo yaliyojengwa bila vibali ambapo mthamini atatoa gharama za ujenzi na mwenye nyumba atalazimika kulipia **2%** yake kama sehemu ya kibali cha ujenzi.
- Kuendelea kutoa elimu kwa walipa kodi ili kuongeza ufahamu wa umuhimu wa kulipa kodi.

4.0 MATUMIZI KWA UJUMLA:

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba, 2017 matumizi ya Halmashauri yamezingatia maeneo ya Matumizi mengineyo **(OC)**, Mishahara ya watumishi **(PE)** pamoja na miradi ya maendeleo.

Kwa matumizi mengineyo yasiojumuisha mishahara ya Ruzuku zimetumika **TZS. 511,386,245.01** sawa na **12%** ya lengo la **TZS. 4,147,540,800.40**.

Kwa upande wa mishahara ya Ruzuku zimetumika **TZS. 2,139,697,392.44** ambayo ni sawa na 11% ya lengo la **TZS. 19,921,585,586.76**

Matumizi yote kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, 2017 ni **TZS. 2,992,209,498.45** ambayo ni sawa na **8%** ya lengo la **TZS. 37,488,175,065.85**

Jedwali Na 2: MUHTASARI WA MATUMIZI KWA UJUMLA KWA KIPINDI CHA SEPTEMBA, 2017.

MAELEZO	MAKISIO 2017/2018	Julai - Agosti 17	Septemba, 2017	Jul - Sept, 2017	%
Matumizi mengineyo (OC)	4,147,540,800.40	279,832,081.13	231,554,163.88	511,386,245.01	12
Miradi ya maendeleo na wafadhili	13,525,235,965.22	135,275,430.72	205,850,430.28	341,125,861.00	3
Mishahara ya Ruzuku (P.E)	19,921,585,586.76	1,426,724,292.44	712,973,100.00	2,139,697,392.44	11
JUMLA	**37,488,175,065.85**	**1,841,831,804.29**	**1,150,377,694.16**	**2,992,209,498.45**	**8**

Angalizo: Miradi viporo ambayo fedha zake zilitengwa mwaka uliopita 2016/2017 na utekelezaji wake unafanyika mwaka huu wa fedha 2017/2018 bajeti yake haikujumlishwa katika jedwali hili ambayo ni **TZS. 826,290,920.43** na matumizi yake ni **TZS. 578,518,341.59** sawa na **70.01%** ya lengo.

5.0 MENGINEYO:

5.1 FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA

Kwa upande wa fedha za mfuko wa barabara kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 bajeti yake **TZS. 2,575,890,000.00** ambapo fedha hizo zitaondolewa katika bajeti yetu na kupelekwa **TARURA** (**Tanzania Rural and Urban Roads Agency**) kufuatia Serikali kuunda taasisi hiyo mpya kuanzia Julai, 2017. Pia Wakala wa barabara za mijini na vijijini imepangiwa pia watumishi kutoka katika Halmashauri yetu ambapo wataalam wa barabara pamoja na wahasibu baadhi yao tayari wamehamishiwa huko

5.2 FEDHA ZA MGAWANYO WA MALI, MADENI NA RASILIMALI FEDHA.

Fedha tulizopaswa kuletewa na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke baada ya mgawanyo wa rasilimali fedha **TZS. 339,392,780.00** bado hazijaletwa japo kamati iliyoundwa kufuatilia jambo hili ikikamilisha kazi yake itakuja na majibu.

HITIMISHO: Taarifa ya mapato na matumizi hadi mwezi Septemba, 2017 bado inaendelea kufanyiwa marekebisho **TAMISEMI.**

Pia Halmashauri inaendelea na zoezi la uthamini wa mali zake kwa kutumia Wataalam wake wa ndani ili kukidhi matakwa ya sheria na vigezo vya kiuhasibu vya Kimataifa kwa hesabu za sekta ya Umma (IPSAS). Hii itaiwezesha Halmashauri kujua thamani halisi ya mali inazomiliki.

Imetolewa na

Stephen E. Katemba
MKURUGENZI WA MANISPAA,
HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI.